



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TANGAZO LA MTIHANI YA USAJILI NA LESENI
DESEMBA, 2023

Wahitimu wote mnatangaziwa kuwa mtihani wa Usajili na Leseni utafanyika tarehe **29/12/2023**, maombi yatafanyika kupitia mtandao kwa kutumia mfumo wa Baraza www.tnmc.go.tz kuanzia tarehe 6/11/2023 hadi tarehe 20/12/2023. Kila mwombaji atatakiwa kujisajili na kulipia kiasi cha Shilingi **150,000/-** kwa wale wanaoomba kufanya mtihani huu kwa mara ya kwanza na Shilingi **75,000/=** kwa wanaorudia.

Waombaji wanaofanya mtihani huu kwa mara ya kwanza, wanatakiwa kuhakikisha wamefanya usaili wa awali (Indexing) kwa mujibu wa kifungu cha 14 (1) cha kanuni za mafunzo. Pia, kuzingatia taratibu zote za maombi ambazo zimeambatanishwa ikiwa ni pamoja na kuweka picha sahihi (Passport Size), kujaza majina sahihi yanayoendana na vyeti vya kufunzu sekondari, kufanya malipo kwa wakati na kuchagua kituo sahihi cha mtihani kati ya vilivyoorodheshwa katika jedwali hapa chini:

SN	KITUO CHA MTIHANI	MKOA	IDADI
1	Taasisi ya Afya na Sayansi Shirikishi - Tandabui	Mwanza	1000
2	Chuo Kikuu cha Kampala	Dsm	1000
3	Chuo Kikuu cha St. John	Dodoma	800
4	Chuo cha Stephano Moshi-Kilimanjaro	Moshi	800
5	Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi -Mbalizi	Mbeya	800
6	Chuo Kikuu cha Katoliki Ruaha (RUCO)	Iringa	700
7	Tabora Polytechnic	Tabora	700

Imetolewa na:


Agnes Mtawa
MSAJILI

02/11/2023